

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu+25526 2782443
Barua pepe: acl.njombe@lands.go.tz
Tovuti: www.lands.go.tz



Kamishna wa Ardhi Msaidizi,
Ofisi ya Ardhi Mkoa,
S. L. P. 776,
NJOMBE.

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb. Na. LD/NJB/3/Vol.III/85

22 Juni, 2023

Kituo cha Uwekezaji Tanzania,
S.L.P. 938,
DAR ES SALAAM.

**YAH: UTHIBITISHO WA UMILIKI NA MATUMIZI YA ARDHI KATIKA SHAMBA
NAMBA 898 LILILOKO NJOMLOLE (HATI Na. 13719 – MBYLR)**

Tafadhali rejea barua yenye Kumb. Na. CA.148/234.01.E/02 ya tarehe 16 Juni, 2023 kuhusiana na somo la hapo juu.

2. Kumbukumbu za Usajili wa Hati zinaonesha kuwa shamba namba 898 lililoko Njomlole Mjini Njombe lenye Hati Na. 13719 – MBYLR linamilikiwa na ALLURE FLOWERS LTD wa S.L.P. 180 Njombe kwa milki ya miaka 66 kuanzia 1/1/1988. Milki hii imewekwa rehani (Mortgage) kutokana na mkopo wa fedha uliotolewa na INDUSTRIALISATION FUND FOR DEVELOPING COUNTRIES. Shamba hili linadaiwa kodi ya ardhi kiasi cha Shilingi 25,372,750.00 kama fomu ya makadirio iliyoambatishwa inavyoonesha.
3. Aidha, ukaguzi uliofanywa uwandani tarehe 22 Juni, 2023 umebaini kuwa shamba hili lenye ukubwa wa Hekta 82.21 kwa wakati huu halina shughuli za kilimo au ufugaji zinazoendelea. Ukaguzi umebaini pia kuwa hakuna mgogoro katika shamba hili.
4. Hivyo, nakuwasilishia taarifa hii kwa hatua zako.

Nakutakia kazi mwema.

F. Kanuti

**KAIMU KAMISHNA WA ARDHI MSAIDIZI
MKOA WA NJOMBE**

NAKALA:

Mkurugenzi wa Mji,
Halmashauri ya Mji Njombe,
S.L.P.577,
NJOMBE.

Mkurugenzi,
Avoafrica Farms Tanzania Limited
S.L.P. 67,
NJOMBE.